# KIRINYAGA COUNTY

# DARASA LA SABA MUHULA WA TATU

PENPLUS KIRINYAGA

## KISWAHILI

***Muda: Saa 1 Dakika 40***

***JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU***

1. *Tumia penseli ya kawaida.*
2. *Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:*
   *(I) JINA LAKO* *(II) JINA LA SHULE YAKO*
3. *Kwa kila swali onyesha jibu sahihi kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndiyo jibu.*

---

***Chagua jibu sahihi kati ya yale uliyopewa kujaza nafasi zilizoachwa.***

Nyuki aliirukia ua __1__ __2__ halua mpaka ikaisha. Alikwenda __3__ ua __4__ __5__ akafanya tena vivyo hivyo. Hatimaye nyuki __6__ kurudi mzingani __7__. Alipofika juu aliyaona maua __8__ yaliyokuwa ng'ambo ya mto __9__ kulikuwa na bustani kubwa zaidi ya mfalme.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. lekundu | B. mwekundu | C. jekundu | D. nyekundu |
| 2. | A. akafyonza | B. akanyonya | C. akanywa | D. akala |
| 3. | A. na | B. mpaka | C. kwenye | D. kwa |
| 4. | A. jingine | B. lingine | C. nyingine | D. kingine |
| 5. | A. nyeupe | B. jeupe | C. mweupe | D. cheupe |
| 6. | A. aliamuru | B. alikamua | C. aliamua | D. alisema |
| 7. | A. yake | B. mwake | C. kwake | D. lake |
| 8. | A. mengine | B. mingine | C. nyingine | D. jingine |
| 9. | A. ambayo | B. ambapo | C. ambamo | D. ambako |

Kijana huyo __10__ vizuri. __11__ kwa kila alilofanya. Hata hivyo, dunia ni rangi rangile. __12__ mtoto wa watu __13__ __14__ kudekezwa kupita kiasi. Kumbe __15__! Hatima yake akawa pwaguzi pale kijijini pao.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. alikua akikua | B. alikuwa | C. alikuwa akikua | D. alikuwa akikuwa |
| 11. | A. aliwajibika | B. aliadhirika | C. alibahatika | D. alighadhabika |
| 12. | A. Maskini! | B. Lo! | C. Kijana | D. Yeye |
| 13. | A. aligura | B. alitota | C. alinuna | D. alipotoka |
| 14. | A. huku | B. na | C. kwa | D. kutokana |

15. A. mui huwa mwema
    B. aliyetota hajui maana ya kutota
    C. Mumunye huharibika ukubwani
    D. damu si katarasa

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

16. Juma alimwamkua Katana "tuonane tena". Katana alimjibu ________

A. chewa
B. inshallah
C. buriani dawa
D. starehe

17. Wanafunzi walisoma kwa kupita mtihani.

Neno <u>kwa</u> limetumika vipi?

A. Kuonyesha sababu
B. Kuonyesha jinsi
C. kuulizia swali
D. kuonyesha "pamoja na"

18. Ni mapambo yapi kati ya haya huvaliwa puani?

A. Hazama, udodi, nyerere
B. Kishaufu, hazama, kikero
C. Kekee, kipini, kishaufu
D. Mapete, kipuli, bali

19. Wangegombana wangekamatwa. Sentensi hii ina maana gani?

A. Waligombana na walikamatwa
B. Hawakugombana na walikamatwa
C. Waligombana na hawakukamatwa
D. Hawakugombana na hawakukamatwa

20. Anayesoma na kusahihisha vitabu na magazeti kabla yachapishwe ni ________

A. mhazili
B. mhasibu
C. mhariri
D. mhandisi

21. Bainisha sifa kutokana na kitenzi <u>cheka</u>.

A. Chekesha
B. Chekea
C. Chekwa
D. Mcheshi

22. ***Tegua kitendawili kifuatacho***

Tik! Tik! kucha kutwa! ________

A. roho
B. gari moshi
C. ndege
D. moyo

23. ***Andika wingi wa sentensi hii***

Afisi ya balozi iliteketea kwa moto.

A. Afisi za mabalozi ziliteketea kwa moto.
B. Maafisi ya mabalozi yaliteketea kwa moto
C. Afisi ya mabalozi yaliteketea kwa moto
D. Maafisi za balozi ziliteketea kwa moto

24. Kizuka ni kwa mjane, kama vile kirukanjia ni kwa ________

A. sayidina
B. beberu
C. kirukamito
D. bwamdogo

25. "Ogopa" katika kauli ya kutendesha ni ________

A. ogofya
B. ogopeka
C. ogopwa
D. ogopea

26. Leo mjakazi amekiandaa chakula kinachonukia ________

A. waa
B. fee
C. fyu
D. nhh

27. ***Tumia O-rejeshi kubadilisha sentensi ifuatayo.***

Mtoto ambaye hujitahidi hufua dafu.

A. Mtoto anajitahidi hufua dafu.
B. Mtoto akijitahidi atafua dafu
C. Mtoto ajitahidiye hufua dafu.
D. Mtoto ambaye anajitahidi anafua dafu

28. Malipo ya hiari ya ujenzi wa taifa ni ________

A. riba
B. arbuni
C. masrufu
D. ushuru

29. Jaza pengo kwa kutumia sifa mwafaka.

Taifa __________ lilikumbwa na janga la njaa.

A. nzima
B. mzima
C. zima
D. kuzima

30. Maana ya msemo "kazi ya shokoa" ni ________

A. kazi ya kushirikiana
B. Kazi ngumu ya kulazimishwa
C. kazi ngumu
D. kazi ya hiari

*Soma kisa hiki kisha uyajibu maswali 31-40.*

Aliondokea dalali mmoja na kondoo wake akielekea mnadani. Mwendo ulikuwa mrefu. Naye alianza kunyemelewa na taashira za uchovu. Alipolemea msituni alichoka zaidi. Kondoo alichoka zaidi ya dalali mwenyewe. Akawa akihema na kutweta kama punda mwenye mzigo mgongoni.

Mara ikatokea ibra. Kiatu kizuri kipya kilionekana kando ya njia. Dalali alitaharuki na kuhaha. "Kiatu chenyewe ni kizuri mno. Lakini ni kimoja tu kitanifaa nini?" Alisema komoyomoyo.

Mara alikitupa chini na kukata shauri kuendelea na safari yake. Baada ya mwendo wa nusu saa tu alikikuta kiatu cha pili. "Lo, salala! Ama kweli, nilifanya ujuha usio na kifani kukiacha kile kiatu cha mguu wa kulia kule njiani!"

Tamaa hutawala nadhari. Na pasipo budi hubidi. Dalali alinuia na kukamia kuwa na viatu vipya vya sudi na bwerere. Potelea mbali hata kama atachelewa kufika mnadani asimwuze kondoo wake. Lakini pana hasara gani mradi atarejea nyumbani na viatu vipya miguuni. Bahati yake. Asiye na bahati habahatishi. Hakudharau kwani mdharau biu hubiuka na hasara humfika mwenye mabezo.

Baada ya kuliwaza moyo, alimfunga kondoo shinani pa mti ndi! Kile kiatu na kijiti cha kuswagia mnyama wake, akavitupa kando ya kondoo. Akatimua mbio kurudi nyuma. Safari hii kwa mbio wala uchovu hakuna. Alipofika kule hakuona kiatu. Njozi au miuja hakuajizi. Akarejea mbio kwa rasilimali yake. Huko nako hakumkuta kondoo, kiatu cha pili wala kijiti. Mazingaombwe ama nini? Hakuamini macho yake. Aliduwaa na kubung'aa.

31. Dalali ni mtu gani?
   A. Mchuuzi wa mnadani
   B. Mwuza kondoo
   C. Mwenye dalili za kuchoka
   D. Mnunuzi wa bidhaa mnadani

32. Dalali na kondoo walichoka kwa sababu ________
   A. jua lilikuwa kali
   B. walikiona kiatu
   C. mwendo ulikuwa mrefu
   D. ya msitu

33. Ibra gani iliyotokea?
   A. Kiatu kilipotea
   B. Dalali alitaharuki na kuhaha
   C. Kiatu kipya kilionekana karibu na njia
   D. Kondoo na kijiti kupotea

34. Kwa nini dalali alikitupa chini kiatu?
   A. Kilikuwa kizuri mno
   B. Kilikuwa nambari yake
   C. Watu wangedhani amezaliwa nacho
   D. Hakuwa na cha pili chake

35. Nilifanya <u>ujuha.</u> Neno hili ni sawa na ________
   A. ujuaji  B. upumbavu  C. ujanja  D. ujuzi

36. Kitendo cha dalali kurudi nyuma mbio kinaonyesha tabia ya ________
   A. haraka  B. hasara
   C. papara  D. busara

37. Neno uchovu hutokana na ________
   A. cheka  B. chokaa
   C. chuki  D. choka

38. Baada ya kukikosa kiatu, dalali ________
   A. aliendelea na safari
   B. alirudi upesi alikomwacha kondoo
   C. alimwuza kondoo
   D. alipoteza kondoo pia

39. Jambo ambalo dalali aliona mazingaombwe ni ____
   A. kupoteza vyote
   B. kuokota kiatu
   C. kukosa kiatu
   D. kupiga mbio

40. Ni dhahiri kuwa ________
   A. tamaa mbele mauti nyuma
   B. mtaka yote hukosa yote
   C. pwagu hupata pwaguzi
   D. akili ni mali

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.***

Teknolojia imeleta mfumo mpya wa maisha kote ulimwenguni. Imekuwa nadra sana kwa watu wa mataifa kutekeleza kazi zao kivyao. Hii ni kwa sababu mitambo ya tarakilishi imeenea kote na matumizi yake si mapya tena. Hali hii imekuwa msukumo mpya wa maendeleo katika nyanja mbalimbali za nchi kama vile biashara, uvumbuzi wa bidhaa mpya viwandani na vyombo vya kuonewa fahari katika makazi ya watu, vikiwemo redio, runinga na majiko.

Kweli dunia nzima imekuwa kijiji tu hivi, mlango wa kwenu unakabiliana na wa kwetu na mawasiliano, mapatano na uhusiano huu kuwa bayana zaidi. Kale, watu walichukua muda mrefu kuandikiana nyaraka zilizochukua miezi kadhaa kufika; siku hizi huduma hii ya shirika la posta na nyingine hapa na pale si kizuizi kikubwa kwa mawasiliano na umuhimu wake umeachiwa uwasilishi wa vifurushi. Watu wengi hutuma ujumbe mfupi pamoja na rununu. Barua pepe nazo ni nyingine ambazo zimeimarisha mawasiliano hasa kutoka mabara, pasi kuwa na gharama kuu kama hapo awali . Kipepesi na mitambo ya umeme vinatumika katika nyanja mbalimbali kote duniani.

Hata hivyo, kila masika yana mbu, nao mbu husambaza malaria. Kupitia vyombo vya habari na mawasiliano, vijana wetu wamechukua hulka za kizungu. Matumizi ya dawa za kulevya, kujivalia nusu uchi na lugha chafu, ni baadhi ya yanayochangia ongezeko la visa vya ubakaji.

Ni kweli kuwa mambo mapya yakija watu hujifunza mengi lakini si yote ambayo huja yana manufaa kwetu.

41. Watu wa mataifa hawawezi kutekeleza shughuli kivyao kwa sababu _____

A. mawasiliano yamekuwa na gharama kuu
B. ulimwengu umekuwa kijiji tu
C. mataifa mengine hayana nguvu za umeme
D. kiwango cha teknolojia kimekuwa sawa kote

42. Neno "nadra" kama lilivyotumika linamaanisha _____

A. kawaida B. mbeleni
C. muhali D. rahisi

43. Ni jambo lipi ambalo limechangia kuunganisha ulimwengu wa sasa?

A. Masomo ya sayansi
B. Ueneaji wa nguvu za umeme
C. Uuzaji wa dawa za kulevya
D. Mawasiliano

44. Semi "kuona fahari" inamaanisha _____

A. kukejeliwa B. kujivunia
C. kuchukizwa D. kubezwa

45. Barua pepe hutumika nyakati hizi kwa sababu zifuatazo isipokuwa _____

A. watu wote duniani wana elimu ya tarakilishi
B. uvumbuzi wa teknolojia mpya
C. huchukua muda mfupi
D. zina gharama ya chini

46. Shirika la posta na simu ni muhimu hususan katika nyanja za _____

A. vifurushi B. elimu ya mawasiliano
C. barua za watu D. matangazo ya bidhaa

47. Kifaa kitumiwacho kutuma nakala ya barua upesi zaidi katika mashirika ni _____

A. rununu B. kidubwasha
C. tarishi D. kipepesi

48. Ni methali ipi kati ya hizi inayoeleza kuwa mambo mapya si mabaya kama asemavyo mwandishi?

A. Mwacha mila ni mtumwa
B. Mgeni njoo mwenyeji apone
C. Vyote ving'aavyo si dhahabu
D. Mla mawe hafi nawe ila mzaliwa nawe

49. Kulingana na ufahamu, matumizi ya mihadarati yanaongeza visa vya _____

A. wizi B. mauaji C. ubakaji D. usalama

50. Kasoro moja ya teknolojia ni _____

A. kuwaelimisha watu
B. kutangaza habari za ulimwengu
C. kueneza habari duniani kote
D. watu kupoteza maadili ya kiasili na kuiga ya kigeni.